yaweze kuendelea kuimarisha miundo yao na uwezo wa usimamizi wa ruzuku kupitia kutekeleza miradi yenye uwezekano wa kuleta mabadiliko mkubwa. Watakaonufaika na programu hii wanatarajiwa kuwa na uwezo mkubwa kuliko wale wanaotekeleza programu ya ruzuku ndogo ndogo (RSG). Kiwango kidogo cha msaada wa kiufundi kitatolewa hususani kwa wale watakaokuwa wanapata ruzuku hii ya kati kwa mara ya kwanza. Ruzuku ya hadi shilingi 105,000,000 kwa miaka 3 zitatolewa. Yaani shilingi 35,000,000 kwa mwaka

Ruzuku Ndogo Ndogo (Rolling Small Grants- RSG)

Ruzuku ya aina hii inatoa fursa kwa vikundi na mashirika (hasa machanga) kwa kutoa ruzuku itakayoyawezesha kujifunza namna ya usimamizi, kujenga utamaduni wa uwajibikaji na kubaini matarajio ya wafadhili. Tunaamini kuwa programu hii inatoa fursa ya pekee kwa mashirika kuendeleza uzoefu wao na uelewa wa kuandika michanganuo ya miradi, usimamizi wa fedha, uwajibikaji na uwazi katika utoaji huduma wa wazi na katika uandaaji wa taarifa za maendeleo na mafanikio, ambayo ndiyo matokeo tarajiwa makubwa ya programu hii. Ruzuku ya hadi shilingi 5,000,000 kwa mwaka, zitatolewa.

Ruzuku ya Kusaidia Usajili (Kwa Vikundi) (Registration Development Grants-RDG)

Ruzuku ya aina hii inalenga kuvisaidia vikundi hai, visivyosajiliwa na vichanga, ili visajiliwe kisheria chini ya sheria ya NGO. Madhumuni ya ruzuku hii ni kusaidia vikundi visivyosajiliwa viweze kusajiliwa na hatimaye viweze kupata ruzuku zinazotolewa na the Foundation kama sera zake zinavyohitaji. Malengo makuu matarajiwa ya ruzuku hii ni kuwa itawezesha vikundi kusajiliwa, kuwa na katiba zao na kufungua akauti za benki kwa ajili ya usimamizi wa fedha hapo baadaye.

Kiasi cha shilingi 200,000 zitatolewa kama mchango wa gharama za kusajili na matayarisho mengine muhimu; pia kwa maandalizi ya nyaraka za kisheria ikiwa ni pamoja na kumlipa mtalaamu atakayesaidia katika zoezi la uandaaji wa katiba kwa ajili ya usajili.

Safari ya Maombi ya Ruzuku



THE FOUNDATION
for Civil Society

THE FOUNDATION
for Civil Society

Haidery Plaza, Ghorofa ya 5,
Mtaa wa Upanga / Kisutu
S. L. P. 7192, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: 022-2138530 / 1 / 2
Nukushi: 022 2138533
Barua Pepe: information@thefoundation-tz.org
www.thefoundation-tz.org

www.milkrection.net

THE FOUNDATION
for Civil Society

Foundation for Civil Society ni Nini

The Foundation for Civil Society ni shirika lisilolenga kupata faida, lilianza kazi zake rasmi Januari 2003 kwa makusudi ya kusaidia ukuaji wa jumuiya na asasi za kiraia nchini Tanzania. Lengo la The Foundation ni kusaidia asasi hizo ili ziweze kushiriki kikamilifu katika michakato ya kupunguza umasikini katika maeneo yao.

The Foundation haina lengo la kuwa mwakilishi au msemaji wa vyama na makundi ya kiraia na kijamii bali kujenga uwezo wa mashirika ya kiraia katika mpango na uratibu wa kiwango cha juu kwa kuzingatia uwajibikaji, uwazi, ubora na matokeo.

Dira

Kuwa mfano endelevu wa ubora ambao unachangia katika kujenga jamii ya makundi ya kiraia yenye ari na ubunifu, yatakayowawezesha wananchi kushiriki katika michakato ya kidemokrasia, kuendeleza haki za binadamu na kuchangia katika kupunguza umasikini na kuinua ubora wa maisha ya Watanzania wote.

Lengo

Kutoa ruzuku na kujengea uwezo asasi za kiraia ili ziwezeshe wananchi, ikiwa ni pamoja na makundi yaliyopembezoni kiuchumi na yale yenye uwezekano wa kuathiriwa zaidi na umasikini (vunerable groups) ili:

- Kupata taarifa na kuelewa haki zao, sheria na sera zinazowalenga
- Kushiriki kikamilifu katika kufuatilia sera na mijadala inayohusu kupunguza umasikini
- Kuchangia katika maendeleo ya jamii na kuibana ipasavyo serikali na sekta binafsi katika masuala yanayohusu maendeleo ya jamii.

Maadili Yetu

The Foundation imejiwekea maadili yafuatayo:

- Haki na Uwazi
- Uadilifu
- Heshima
- Ubora
- Kujifunza na Kujiendeleza

Malengo yetu ya Jumla

Lengo la the Foundation ni kuimarisha uwezo wa makundi na asasi za kiraia kushiriki katika zoezi zima la kupunguza umasikini nchini, kama ilivyoelezwa katika sera za serikali ya Tanzania. Uimarishaji huo unafanywa na The Foundation kupitia programu za kujenga uwezo wa kiutendaji na pia kupitia utoaji wa ruzuku za fedha kwa asasi na vikundi vya kiraia katika mikoa yote Tanzania.

Maeneo Tunayoyapatia Ruzuku

Utoaji wa ruzuku wa Taasisi hii unalenga kwenye maeneo (thematic areas) makuu manne:

- Ushiriki wa wananchi katika masuala yanayohusu sera, Utungaji, uchambuzi, tathmini na ufuatiliaji wake.
- Harakati zinazolenga kuhimiza utawala Bora
- Kuimalisha shughuli za ushawishi na utetezi
- Ujenzi wa mitandao ya kiusalama kwa ajili ya makundi yaliyokatika hatari ya kufukarishwa na kuathiliwa na umasikini ili yaweze kupenyeza hoja zao kwa jamii na vyombo husika (watoto, wajane, wazee au watu wenye kusumbuliwa na magonjwa ya muda mrefu, wasio na ajira nk)

Aina ya Ruzuku Tunazozitoa

Hivi sasa, The Foundation for Civil Society inatoa aina nne za ruzuku za fedha;

- Ruzuku Ndongondogo,
- Ruzuku za Kati
- Ruzuku Kubwa
- Ruzuku ya Kusaidia Usajili

Aina za ruzuku na tarehe za mwisho za kuwasilisha maombi. *(angalia jedwali hapa chini)*

Jumuiya au Asasi zinazoweza kutuma maombi ya ruzuku

- Asasi Zisizo za Kiserikali (NGOs)
- Asasi za Kijamii (CBOs)
- Vyama vya Kiutaalamu
- Vyama vya Wafanyakazi
- Vyama vya ushirika na biashara katika ngazi ya jamii
- Mashirika au Vikundi vya Wanahabari
- Mashirika ya Kidini.

Na kama

- Asasi yako imesajiliwa Tanzania Bara na/au Zanzibar
- Asasi yako imeanzishwa kwa madhumuni ya hisani (si kuzalisha faida)
- Una katiba au sheria ndogondogo halali zinazotambulika zinazoyaeleza madhumuni ya asasi yako na jinsi unavyoiendesha
- Asasi yako ina akaunti ya benki inayoendeshwa na watia saini zaidi ya mmoja
- Walau mwaka mmoja umekwisha tangu asasi yako ilipoanzishwa na kuanza kazi

Ruzuku Kubwa (Strategic Grants)

Ruzuku hii inalenga kuyawezesha mashirika yaliyojiimarisha kuomba ruzuku kwa:-

I. Kuendeleza miundo mbinu na uwezo wa shirika husika.
II. Kuanzisha na kukamilisha miradi mipya iliyotayarishwa vizuri, ambayo inafikia malengo ya kimkakati ya mashirika husika.
III. Gharama za msingi ambazo ni muhimu kwa kuendeleza na kuendesha shirika lao, kuwawezesha kukidhi malengo yaliyopangwa na shirika husika.
IV. Kukuza uwezo wa mashirika kuanzisha na kukamilisha miradi iliyoandaliwa vizuri ambayo inakidhi malengo ya kimkakati ya mashirika hayo.
V. Kuboresha ubunifu kwenye sekta ya jumuiya za kiraia, kwa mfano miradi inayotumia njia mpya na bora zaidi za namna ya kufanya kazi kwenye jumuiya za kiraia (CSO), asasi zisizo za kiserikali (NGO) na vikundi vya kijamii (CBO).

Katika kila eneo lengwa kwa ajili ya ufadhili lililotajwa juu, matokeo yenye kuonyesha dhahiri mabadiliko ya muda mrefu (outcome and long term impact) lazima yawe bayana. Ruzuku za hadi shilingi 300,000,000 kwa miaka mitatu zitatolewa. Yaani shilingi 100,000,000 kwa mwaka.

Ruzuku ya Kiwango cha Kati (Medium Grants)

Ruzuku ya aina hii inatoa fursa kwa ajili ya mashirika yanayoendelea, yenye uzoefu wa kusimamia ruzuku, ili

Aina za Ruzuku	Kiwango cha Juu kwa Mwaka	Kiwango cha Juu cha muda wa Ruzuku	Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha Maombi	Mwombaji atajulishwa katika muda wa	Kama imekubaliwa, fedha zitatolewa katika muda wa
Ruzuku Kubwa	Shs 100 milioni	Miaka 3	Muda wowote	Majuma 16	Majuma 24
Ruzuku ya Kati	Shs 35 milioni	Miaka 3	Februari 1 Juni 1 Oktoba 1	Majuma 8	Majuma 16
Ruzuku Ndogondogo	Shs 5 milioni	Mwaka 1	Aprili 1 Julai 1 Septemba 1 Novemba 1	Majuma 8	Majuma 16
Ruzuku ya Usajili	Shs 200 elfu	Mara moja	Muda wowote	Majuma 8	Majuma 16

www.thefoundation-tz.org